ZURA
Zanzibar Utilities Regulatory Authority

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR**

08/08/2025

**TAARIFA KWA UMMA JUU YA BEI ZA MAFUTA KWA MWEZI AGOSTI 2025**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) inatangaza Bei za Mafuta kwa Mwezi Agosti 2025 zitakazoanza kutumika rasmi kuanzia Siku ya **Jumamosi Tarehe 09/08/2025**.

Mamlaka hupanga bei kwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- Wastani wa mwenendo wa mabadiliko ya bei za Mafuta Duniani (Platts Quotations).
- Gharama za uingizaji Mafuta katika bandari ya Tanga.
- Gharama za Mabadiliko ya Fedha za kigeni zinazotumika kununulia mafuta.
- Gharama za Usafiri, Bima na 'Premium' hadi Zanzibar.
- Kodi na Tozo za Serikali.
- Kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na reja reja.

Bei za mafuta kwa mwezi Agosti, 2025 ni kama zifuatazo:

| AINA YA MAFUTA | BEI YA MWEZI JULAI, 2025 (TZS/LITA) | BEI YA MWEZI AGOSTI, 2025 (TZS/LITA) | TOFAUTI (TZS/LITA) | TOFAUTI ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| PETROLI | 2,996 | 2,978 | -18 | -0.60 |
| DIZELI | 2,907 | 3,076 | 169 | 5.81 |
| MAFUTA YA TAA | 3,000 | 3,000 | - | - |
| MAFUTA YA NDEGE | 2,370 | 2,421 | 51 | 2.15 |

Sababu za mabadiliko ya Bei za mafuta kwa mwezi Agosti, 2025 zimetokana na mabadiliko ya bei za ununuzi katika soko la dunia, gharama za uagizaji wa bidhaa za mafuta kutoka soko la dunia hadi kufika Zanzibar pamoja na fedha za kigeni.

Aidha, Mamlaka inawahimiza Wananchi kununua Mafuta katika Vituo halali vya Mafuta na kudai Risiti za Kielektroniki kila wanaponunua Mafuta.

**IMETOLEWA NA KITENGO CHA UHUSIANO (ZURA)**

MAMLAKA YA UDHIBITI HUDUMA ZA MAJI & NISHATI
ZURA
Zanzibar Utilities Regulatory Authority
P.O.Box 2238
★ ZANZIBAR ★